



TANGAZO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI



FURSA YA MIKOPO KWA VIJANA TOKA OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU KUPITIA MFUKO WA MAENDELEO YA VIJANA KAMA IFUATAVYO;

LENGO LA MFUKO WA MAENDELEO YA VIJANA

Kuinua na kuzalisha nafasi za ajira kupitia mikopo yenye masharti nafuu kwa nia ya kusaidia ukuaji wa biashara endelevu kwa vijana.

WAOMBAJI WANAOSTAHILI

Fursa ya mfuko huu ni kwa vijana wote wa kitanzania ambao wana biashara/ miradi au wana wazo la biashara linalokusudiwa kutekelezwa. Walengwa wa mikopo hii ni kama ifuatavyo;-

- i) Kijana binafsi mwenye umri wa miaka 18 – 35 atakayekuwa ameorodheshwa kwenye rejista ya vijana ya Wilaya ii) Vikundi vya vijana iii) SACCOS za vijana iv) Kampuni/ viwanda vinavyomilikiwa na vijana.


UTARATIBU WA KUOMBA

Waombaji watatakiwa kujaza fomu ya maombi inayopatikana bure katika ofisi za Halmashauri (KDC). Fomu ya maombi itatakiwa kuambatishwa na nyaraka zifuatazo;-


- i. Nakala ya cheti cha jina la biashara/ kampuni/ kikundi/ SACCOS au usajili wowote rasmi unaotambulika.
- ii. Nakala ya leseni ya biashara (inapowezekana)
- iii. Nakala ya moja ya vifuatavyo;- kitambulisho cha Taifa, hati ya kusafiria, leseni ya udereva, kitambulisho cha mpiga kura na cheti cha kuzaliwa kilichothibitishwa.
- iv. Barua ya utambulisho toka kwa Mtendaji wa kijiji.
- v. Nakala ya namba ya utambulisho wa mlipa kodi - TIN (inapowezekana)
- vi. Mpango wa biashara au andiko la mradi.
- vii. Nakala ya katiba.
- viii. Wasifu wa waombaji (CVs).
- ix. Nakala ya cheti cha ujuzi (Kama kipo).
- x. Akaunti namba ya kuwekea mkopo.
- xi. Taarifa ya benki - Bank statement (inapowezekana)

Fomu za maombi zitakazojazwa kwa ukamilifu na kuambatishwa na nyaraka tajwa hapo juu ziwasilishwe kwenye ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji kupitia kwa Afisa vijana kwa ajili ya kufanya tathmini na hatua zaidi kabla ya kupelekwa Mkoani.

Limetolewa na:


Kastori G. Msigala
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
MOSHI

30/11/2022


Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya
Moshi